**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**USHAURI KWA WASAFARI (Na. 1 wa tarehe 23 Machi, 2020)**

# TAARIFA YA HALI YA UGONJWA WA COVID-19 NCHINI TANZANIA

Kutokana na mlipuko wa ugonjwa wa Homa ya Mapafu unaosababishwa na Virusi vipya vya Corona (COVID-19) unaoendelea kusambaa kutoka kwa mtu hadi mtu ulimwenguni kote, huku Tanzania ikiwa ni mojawapo ya nchi iliyoripoti kuwa na watu wenye maambukizi ya Virusi hivyo, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania imeendelea kuchukua hatua za ziada ili kudhibiti kuenea kwa virusi hivyo nchini.

Hatua zilizochukuliwa kuanzia Machi 23, 2020 ni kwamba, wasafiri wote watakaoingia ndani ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania wanapaswa kuzingatia maelekezo yafuatayo:

- Wasafiri wote (raia wa kigeni na Watanzania wanaorejea nchini) kutoka nchi zilizoathirika zaidi na ugonjwa wa Corona (COVID-19) watalazimika kutengwa (Mandatory Isolation) kwa muda wa siku 14 katika maeneo yatakayoainishwa na Serikali kwa gharama zao.
- Wasafiri wote wanaoingia nchini watatakiwa kujaza fomu za ufuatiliaji wa masuala ya afya (Health Surveillance Form) ndani ya ndege au vyombo vingine vya usafiri na kuziwasilisha kwenye dawati la Timu ya Afya mipakani (Port Health Authorities) watakapofika nchini.
- Wasafiri wote watakaoingia nchini watafanyiwa ukaguzi wa kina (additional screening) ikiwa ni pamoja na kuchukuliwa vipimo vya haraka (COVID-19 rapid test).
- Wasafiri wote watakaoingia nchini watajulishwa kuhusu maeneo yaliyoandaliwa kwa ajili ya kutenga wasafiri (Isolation centres) pamoja na gharama za matunzo na utaratibu wa kufika kwenye maeneo hayo.
- Baada ya karantini ya siku 14, msafiri ambaye hatakuwa na maambukizi ya ugonjwa wa COVID-19 ataruhusiwa kutoka na atatakiwa kuacha maelezo binafsi kwa ajili ya ufuatiliaji wa ziada endapo kutakuwa na uhitaji huo.
- Watu wote wanaoishi nchini Tanzania wanashauriwa kutosafiri kwenda katika nchi zilizoathirika na COVID-19 endapo hakuna ulazima wa kusafiri.
- Endapo msafiri atapata dharura yoyote ya afya, atatakiwa kupiga simu ya bure **(Health Emergency)** namba 199.

**NB**: Ushauri huu kwa wasafiri utaendelea kuboreshwa mara kwa mara kutokana na mabadilliko ya hali ya ugonjwa hapa nchini. Utekelezaji wa hatua hizi mpya utaanza mara moja kuanzia tarehe 23 Machi, 2020.

**UMMY A. MWALIMU (MB),**
**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII**
**JINSIA, WAZEE NA WATOTO**
**23.03.2020**